

# CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO



## TAARIFA KWA UMMA

SHAMRA SHAMRA ZA IJA BONANZA 2019

CHACHU KWA AFYA NA BURUDANI

Desemba 7, 2019 IJA - Lushoto

Katika kuadhimisha sherehe za Uhuru, Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) kikiongozwa na **Mkuu wa Chuo Mhe. Jaji Paul F. Kihwelo (PhD)** ambaye pia ni Mgeni Rasmi wa tukio hili kinatarajia kufanya Bonanza la Wafanyakazi Chuoni ambapo mambo mbalimbali yanatarajiwa kufanyika katika siku hiyo.

Bonanza hili ni fursa adhimu kwa Watumishi wa Chuo kukutana pamoja katika michezo mbalimbali kwa lengo la kuleta hamasa ya kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao sambamba na kutathimini mambo mbalimbali katika mwaka unaokwisha.

Safari hii tukio hili la aina yake litahusisha taasisi kadhaa zilizoalikwa ili kuleta hamasa, kuongeza ushindani na kuleta chachu kwa washiriki. Mionganini mwa taasisi alikwa ni pamoja na Mahakama ya Tanzania Kanda ya Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Polisi Wilaya ya Lushoto, Jeshi la Magereza Wilaya ya Lushoto, na Chuo cha Mabugai.

Akizungumza na wahamasishaji wa timu mbalimbali katika Bonanza hilo Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi Bw. Juma Mshana alisema;

*"Kama yalivyo matukio mengine, Bonanza hili limelenga kuwakutanisha watumishi wa taasisi zilizoalikwa ili kujenga mahusiano mema sambamba na kuchochea ushindani baina yao katika michezo mbalimbali iliyoadaliwa ikiwemo kuhimiza umuhimu wa kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zetu ili kuweza kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi"*

Aidha katika tukio hili zoezi la upimaji litakuepo, ikiwemo Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa hiyari linatarajiwa kufanyika ili kutoa fursa kwa washiriki kuweza kupima afya zao na kupata ushauri nasaha. Sambamba na upimaji wa afya kutakuwa na zoezi la uchangiaji damu salama kwa ajili ya wagonjwa katika hospitali yetu ya Wilaya ya Lushoto zoezi ambalo litaratibiwa na madaktari kutoka hospitali ya Wilaya.

**Nyote Mnakaribishwa**

**Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano IJA**

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto,

S.L.P. 20 Lushoto

Simu: 255-27-2660133

Barua pepe: [info@ija.ac.tz](mailto:info@ija.ac.tz), [pro@ija.ac.tz](mailto:pro@ija.ac.tz)

Tovuti: [www.ija.ac.tz](http://www.ija.ac.tz)